



Taarifa Kwa Vyombo Vya Habari

Warsha ya kuanzishwa kwa Mradi wa Pamoja wa Uwezesaji wa Vijana wa Kike na Wanawake Vijana kupitia Elimu.

23-24 Mai 2017

Protea Hotel, Courtyard, Dar es Salaam

UNESCO, UNFPA na UN Women wameandaa kongamano linalowaleta pamoja viongozi kutoka wizara mbalimbali na wilaya tano, yaani Ngorongoro kutoka mkoani Arusha, Kasulu mkoani Kigoma, Sengerema Mwanza, na Micheweni na Mkoani kutoka Pemba, kujadiliana na kupanga mikakati ya namna bora ya kuwawezesha wasichana na wanawake vijana katika wilaya husika kupata elimu katika kipindi cha miaka minne ijayo.

Kongamano hili linalenga kuzindua mradi wenye thamani ya dola za Kimarekani milioni tano unaofadhiliwa na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Korea (KOICA) kupitia UNESCO. Mkutano huu utawezesha wilaya lengwa kutafakari juu ya vikwazo vya elimu kwa wasichana katika maeneo yao na kubuni mikakati mbalimbali ya kukabiliana navyo ili wasichana wapate fursa ya kujiendeleza kielimu na kukuza fursa ya kuwa raia bora zaidi.

Mradi huu ni sehemu ya mpango wa ulimwengu kupitia mashirika ya UNESCO, UNFPA na UN Women kwa ajili ya kuwawezesha wasichana kupitia elimu uliozinduliwa katika nchi sita duniani kote. Awamu ya kwanza inalenga nchi tatu, yaani Mali, Nepal na Tanzania na ulisainiwa mwishoni mwa mwaka 2016. Wizara ya Elimu, Sayansi na Mafunzo ya Ufundi; Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; na Wizara ya Katiba na Sheria zitaratibu mradi huu kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa niaba ya Umoja wa Mataifa nchini Tanzania, Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi, na Utamaduni (UNESCO) linabeba jukumu la kuratibu mradi huo, na kuutekeleza kwa pamoja na UNFPA na UN Women.

Tukio hili litawezesha uteuzi wa jamii na shule lengwa, kwa kuzingatia idadi ya watu katika wilaya na hali za kijamii na kiuchumi, kutengeneza dira kwa kila wilaya husika na kubainisha watu maalum katika ngazi ya wilaya ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa mradi.

Mradi huu unatarajiwa kuwafaidisha moja kwa moja takribani wasichana na wanawake vijana 8,000 walioko mashuleni na wasichana 600 walioko nje ya shule, kwa kuwapatia fursa ya kuimarisha ujuzi wao wa msingi, ufundi na ujuzi wa kawaida ambao utawawezesha kuwa raia bora katika nchi yao na ulimwengu kwa ujumla ikiwa ni pamoja na kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya Tanzania.

Malengo ya mradi huu yatafikiwa kwa kupitia njia ya kukuza mbinu za pamoja kati ya sekta na taasisi mbalimbali kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma kwa wasichana na wanawake vijana, kuhamasisha jamii kupinga vitendo viovu kama ndoa za utotoni na ukeketaji pamoja na kutoa fursa kwa wasichana vijana walioacha shule au ambao wamekosa elimu rasmi.

Kongamano hili litarasimishwa na Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk Leonard Akwilapo; Mkurugenzi wa KOICA Tanzania, Mr Joonsung Park; Mwakilishi Mkazi wa UNESCO, Bi Zulmira Rodrigues; Mwakilishi wa UNFPA, Dk Hashina Begum, na Afisa Mwakilishi UNWOMEN, Bi Hodan Addou. Kongamano litafanyika katika ukumbi wa Protea Hotel, Courtyard. Tarehe 23 - 24 Mei 2017.

Habari zaidi kuhusu kazi zinazofanywa na UNESCO kuhusiana na elimu zinapatikana katika <http://www.unescodar.or.tz>

Mawasiliano:

UNESCO Dar es Salaam, Tanzania | Mairead de Faoite| +255 769 626 794|
m.defaoite@unesco.org